# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**10/03/2023**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imepokea Kibali cha Ajira ya Mkataba wa Mwaka Mmoja chenye Kumb. Na. FA.170/374/01 "A"/136 cha Tarehe 15 Februari, 2023 kwa Kada mbalimbali kutoka kwa Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Hivyo Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni anakaribisha maombi ya nafasi za Ajira ya Mkataba wa Mwaka mmoja kwa Watanzania wenye sifa kama ilivyoainishwa kwa kila kazi hapa chini:-

## 1.0 MHANDISI DARAJA LA II – Nafasi nane (8)

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Shahada / Stashahada ya Juu ya Uhandisi kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani za Uhandisi.

### 1.2 KAZI/MAJUKUMU YA KUFANYA

i. Kufanya kazi chini ya uangalizi wa Mhandisi aliyesajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi ili kupata uzoefu unaotakiwa.
ii. Kufanya ukaguzi wa Barabara, Madaraja na Majengo mbalimbali.
iii. Kuchunguza vyanzo vya ajali barabarani.
iv. Kufuatilia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Ujenzi wa Barabara na Majengo.
v. Kutayarisha Bajeti ya Mwaka ya Ujenzi na Matengenezo ya Barabara, Madaraja na Majengo
vi. Kusimamia na kuratibu kazi za Barabara / Madaraja na Majengo zinazotolewa na Makandarasi

### 1.3 MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara wa Serikali TGS.**E.1**

## 2.0 MSANIFU MAJENGO DARAJA LA II – Nafasi tatu (3)

### 2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Shahada / Stashahada ya Juu kutoka Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani zifuatazo:- Architecture, Building Design, Architectural and Building Engineering Technology, Landscape Architecture and Planning, Architectural Technology, Naval Architecture, ArchitecturalEngineering, Construction Management, Conservation Architecture, Interior Design au fani nyingine zinazofanana na hizo

### 2.2 KAZI/MAJUKUMU YA KUFANYA

i. Kuandaa Mpango wa mahitaji ya kiufundi na bajeti ya mradi husika
ii. Kukagua eneo la mradi na kuandaa taarifa
iii. Kushauri kuhusu uteuzi wa makandarasi na wataalamu wengine wa mradi
iv. Kufanya upekuzi yakinifu wa mradi
v. Kufanya tathmini ya athari za kimazingira ya mradi husika
vi. Kuandaa michoro ya awali (outline proposals) na michoro yenye mahitaji kamili ya mradi (scheme designs)
vii. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa eneo la miradi (Regular site visits)
viii. Kushauri kuhusiana na miliki ya majengo ya kale
ix. Kukagua majengo ambayo yamekamilika kujengwa kwa madhumuni ya kutoa ushauri ili jingo liweze kupatiwa hati ya kutumika (Certificate of Occupancy)
x. Kufanya kazi nyingine zinazoendana na fani yake kwa kadri atakavyopangiwa na mkkuu wake wa kazi.

### 2.3 MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara wa Serikali TGS.**E.1**

## 3.0 MKADIRIAJI MAJENZI DARAJA LA II – Nafasi sita (6)

### 3.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Shahada / Stashahada ya Juu kutoka Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani zifuatazo: Construction Management, Building Surveyor, Building Economics, Quantity Surveying au fani nyingine zinazofanana na hizo.

### 3.2 KAZI/MAJUKUMU YA KUFANYA

i. Kutoa ushauri kuhusu makadirio ya gharama za awali za ujenzi.
ii. Kuandaa Mipango na Makisio ya gharama za ujenzi na zabuni (Bill of Quantity.
iii. Kukagua na kutathmini kazi inayoendelea kwa ajili ya malipo katika hatua mbalimbali za mradi
iv. Kuandaa na kutathmini gharama za kazi za ziada zinapotokea (Evaluation of Variations)
v. Kuandaa Mahitaji ya Miradi ya Ujenzi (Project resources) na
vi. Kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri wako

### 3.3 MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara wa Serikali TGS.**E.1**

## 4.0 FUNDI SANIFU DARAJA LA II – Nafasi kumi na tatu (13)

### 4.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye mojawapo ya sifa zilizotajwa hapa chini:-

i. Wahitimu wa Kidato cha sita na kufuzu Mafunzo ya ufundi ya miaka miwili kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali katika moja ya fani za Ufundi.
ii. Wahitimu wa Kidato cha Nne na kufuzu Kozi ya Ufundi ya miaka mitatu kutoka Vyuo vya Ufundi vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani ya Ufundi.
iii. Wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Hatua ya I kutoka Chuo cha Ufundi kinachotambuliwa na Serikali
iv. Wenye Stashahada ya Kawaida katika Fani ya Ufundi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

### 4.2 KAZI/MAJUKUMU YA KUFANYA

i. Kufanya kazi za Ujenzi wa kuta za nyumba na kupaka rangi na kufunga mabomba.
ii. Kuchonga vifaa vya nyumba za Serikali ikiwa ni pamoja na Samani "Furniture"
iii. Kufanya kazi za upimaji (survey) wa Barabara, Majengo na Mifereji kama atakavyoelekezwa.
iv. Kuwapangia kazi Mafundisanifu wasaidizi na kuhakikisha wanamaliza kama ilivyopangwa.

### 4.3 MSHAHARA:

Ngazi ya Mshahara wa Serikali TGS.**C.1**

**NB: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI:-**

i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania ambao hawazidi umri zaidi ya miaka 45 na hawapungui umri wa miaka 18,

ii. Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) wenye mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu.

iii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya *TANGAZO LA KAZI.*

iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo

   a) Shahada/ Stashahada ya Juu/ Stashahada/Astashahada/Cheti cha Utaalam kulingana na sifa za nafasi husika.

   b) Cheti cha mtihani wa kidao cha nne au sita,

   c) Cheti cha kuzaliwa.

v. Hati ya matokeo ya kidato cha nne (Result slip) haitafanyiwa kazi.

vi. "Transcript" ambayo haikuambatanishwa na cheti haitafanyiwa kazi.

vii. Kuwasilisha vyeti vya kughushi na maelezo mengine itasababisha kuchukuliwa hatua za kisheria.

viii. Watumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.

ix. Waombaji ambao walistaafu kazi kwa sababu yoyote ile hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.

x. Waombaji waonyeshe wadhamini wawili na mawasiliano yao, anuani na namba za simu.

xi. Waombaji wenye vyeti ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya ufundi la Taifa (NACTE) na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).

xii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au kiingereza.

xiii. Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri – www.Kinondonimc.go.tz

xiv. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **27 Machi, 2023** saa tisa na nusu (**9:30**) Alasiri.

xv. Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Manispaa.

xvi. Maombi yatakayoletwa kwa mkono hayatapokelewa na hayatafanyiwa kazi

xvii. Maombi yote yatumwe kwa Anuani ainishwa hapa chini :-

**Mkurugenzi wa Manispaa,**
**Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni,**
**S.L.P. 31902,**
**DAR ES SALAAM.**

*Hanifa S. Hamza*
**MKURUGENZI WA MANISPAA**